

**“ULEMAVU BARANI AFRIKA”**  
**EPISODE 4: "ULEMAVU SIO KUTOWEZA"**

**AUTHOR: Chrispin Mwakideu**

**EDITORS: Andrea Schmidt, Aboubakary Liongo**

**List of characters / Episode 4:**

**MSIMULIZI**

**SCENE ONE: OUTSIDE CHITOTO'S HOMESTEAD**

- Tofa (mke, 40)
- Fagilio (mume, 42)

**SCENE TWO: AT OLUANDA'S SCHOOL COMPOUND**

- Oluanda (mume, 18)
- Mwanagenzi (mume, 17)
- Kangwa (mke, 18)

**SCENE THREE: TOFU'S VISIT TO THERESA**

- Tofa (mke, 40)
- Theresa (Mke, 65)
- Zabibu (mke, 15)

**SCENE FOUR: AT THE HEADTEACHER'S OFFICE**

- Oluanda (mume, 18)
- Bi. Nina (mke, 45)

### **UTANGULIZI:**

Nakusalimu na karibu tena katika kipindi chetu cha nne tamthilia ya redio kwa isimu ya, “**Ulemavu barani Afrika**”, hadithi kuhusu jamii inayotengwa mno Afrika. Katika kipindi kilichopita, Oluanda alirudi nyumbani kutoka hospitali baada ya kupoteza mguu wake, lakini mienendo yake ikabadilika kabisa. Sahibu yake Magoto hakuridhisha jinsi alivyofanya alipomuona Oluanda na magongo. Kangwa, msichana ambaye anamezewa mate na vijana wote kijijini akiwemo pia Oluanda mwenyewe, tulishuhudia akiregeshwaa mlangoni na Oluanda, na kumshangaza mamake zaidi. Hadithi hii itatuabirisha hadi ngama ipi? Oluanda alitaka sana kurudi shule na baada ya majuma kadha kupita akiuguza kidonda alipewa ruhusa na Dkt Esther, kuwa yu tayari kurudi shule. Tofa alitaka sana kwenda kumsimanga babake Chitoto na asubuhi ile ilikuwa wakati muafaka kumvyogea kwake.

## **SCENE ONE: OUTSIDE CHITOTO'S HOMESTEAD**

- 1. SFX :** **BRUSHING OF TEETH AND GURGLING WITH WATER, OUTSIDE YARD AMBIENCE**
- 2. TOFA:** Fagilio! (**angry**) wewe na mwanao mutualipa kwa maovu muliyomtendea mwanangu...
- 3. SFX:** **GURGLED WATER SPAT ON GROUND**
- 4. FAGILIO:** Tofa! Kwani ni wewe? haiwezekani!... kwani una nini na mwanangu?
- 5. TOFA:** Ala, unajifanya huelewi sio? Najua mulilokusudia. Wivu, unaona wivu kwa sababu mwanangu yuko bora ki masomo kuliko wako! Basi sasa mushamlemaza lakini ulemavu sio kutoweza. Leo amerudi shule. ndio! Na guu moja lakini akili yake yafanya kazi sio nazi suke kama hiyo ya mwanao!...hukufaulu basi!
- 6. FAGILIO:** (**sarcastic**) Kumbe walevi kijiji hiki tu wengi si haba. Sasa perepere hizi zote ni za nini? Mwanamke akili yako ni timamu?
- 7. TOFA:** (**angry**) Endelea kunifanya mzaha, lakini tutaona mzaha wako utakufikisha wapi. Haya hayaisha! Malipo ni hapa hapa duniani.

- 8. FAGILIO:** Kulipa nini? Hunidai hata hela ya tundu!  
Kwanza ikizidi una deni langu la pombe  
nilikwambia usije hapa bila ya chupa ya  
pombe....
- 9. SFX:** **HURRIED FOOTSTEPS WALK AND FADE AWAY**
- 10. FAGILIO:** Tofa simama! Hebu rudi hapa! (**to himself**)  
Kwani dunia imedilika hivi au ni ulevi wangu?  
Sikumbuki mwanamke akimpa mwanamume  
mgongo anapozungumziwa .
- 11. MSIMULIZI:** Kuna methali isemayo, uchungu wa mwana  
aujuae mzazi... Tofu alikua mmoja wa wazazi hao. Lakini  
atayaweza yanayokuja? Sasa tupige darubini kwa Oluanda  
tujue kunaendelea nini hivi ambavyo amerudi shule. Wanafunzi  
wenzake hawakumpa amani.
- SCENE TWO : AT OLUANDA'S SCHOOL COMPOUND**
- 12. SFX: SCHOOL BELL RINGS; SCHOOL YARD AMBIENCE;  
STUDENTS CHATTERING**
- 13. MWANAGENZI :**(mockingly) Wewe Oluanda! Kengele  
imepigwa! Kimbia! La sivyo utafika darasani  
kama masomo yameisha...
- (Huge laughter from some students)**

14. **OLUANDA:** (**angry**) Musiniudhi au sivyo nitawashtaki kwa mwalimu mkuu.
15. **MWANAGENZI :**(**chant**) Oluanda, Mlemavu! Oluanda kiwete!
16. **SFX:** **CRUTCHES MOVING FAST ON FLOOR**
17. **OLUANDA:** (**raving angry**) Unafikiri utanichokoza nikuwache..subiri tupambane kama wewe ni mume!..njoo!
18. **SFX:** **STUMBLING AND FALLING DOWN**  
**(Laughter continues)**
19. **MWANAGENZI:** Maskini Oluanda, sasa ndio ushachelewa kabisa!
20. **KANGWA:** Oluanda! (**calls out**) Oluanda! Umeumia?  
Acha nikusaidie kuenuka.  
**(Act out being lifted out)**
21. **OLUANDA:** (**Embarassed**) Eeeee...asante Kangwa.  
Nenda nisikucheleweshe....
22. **KANGWA:** Sina haraka, na sioni shida kutembea na wewe. Kwanza saa hizi hatuna somo lolote.  
Marafiki zako wako wapi?

23. **OLUANDA:** Gani hao? Kama unamaanisha kina Chitoto, Magoto na Karemi basi hao kuwaita marafiki zangu ni kuharibu msamiati, tafuta jina jengine la kuwaita. Wote wameniacha,, hata afadhali Karemi huja kunitembelea kila wakati..
24. **KANGWA:** Pole sana, hata hivyo ni vyema sana umerudi shule. Utamchukulia hatua ye yeyote Chitoto? Alikuacha pale kama umeumia.. nusura upatwe na mauti..
25. **OLUANDA:** La, sio makosa yake. Makosa yalikuwa yangu mia fil mia. Najuta, naomba mambo yangelirudi kama zamani.. Nawatamani sana marafiki zangu....
26. **MSIMULIZI:** Wengi wa watu wenye udhaifu wa kimaumbile hutengwa sana katika maisha ya kawaida; marafiki na hata ndugu na jamaa zao huona aibu kuhusishwa nao. Kangwa alikua tofauti...lakini huo ulikua mwanzo tu. Kule nyumbani Tofa alihitaji mtu wa kuzungumza naye na aliamuwa kumtembelea jirani yake, Theresa. Tusikilize busara au umbea uliompeleka.

### **SCENE THREE: TOFA'S VISIT TO THERESA**

27. **SFX:** FOOD FRYING IN PAN
28. **TOFA:** Nakwambia.. Fagilio na kijana wake ni lazima waadhibiwe. La sivyo, watazorotesha maisha

ya watoto wengi humu kijijini. Hatujui ni yupi waliyemlenga baada ya Oluanda.

29. **THERESA:** Nakubaliana nawe, lakini wataadhibiwa vipi? Haki itatendeka vipi? Unajua vyema kuwa jamii yetu haimsikizi mwanamke..
30. **ZABIBU:** Chitoto anafaa kumuomba msamaha Oluanda kwa kumuacha akiwa katika hali mbaya.
31. **TOFA:** Nani ! Shetani yule aombe mtu msamaha?
32. **ZABIBU:** Basi kama ni shetani apelekwe jehanamu ! makao ya shetani ni jehanamu sio huku, si ndio nyanya?
- ( Laughter from Tofa and Theresa)
33. **THERESA:** Zabibu, hebu tupishe tuendelee na mazungumzo. Chakula kikiiva nitakuita.
34. **ZABIBU:** Ndio. nyanya. Basi naenda nje?
35. **THERESA:** Sawa, lakini usikawie sana. Jua ni kali saa hizi. Usisahau unakazi za shule pia...
36. **SFX: WOODEN STOOL DRAGGED ON GROUND**
37. **TOFA:** Kazi za shule? Nilifikiri Zabibu haendi shule.

38. **THERESA:** Baada ya kusundugwa na wenzake, nilimtoa shule za kawaida, siku hizi anasoma ngumbaru, zile shule za jioni. Haya nieleze kuhusu Oluanda? Si amehamaki sana sasa?
39. **TOFA:** Umejuaje ? au Karemi amekueleza yaliotokea hospitali?
40. **THERESA:** Hapana. Hata mimi ninayo masaibu yaliyonipata. Nitakueleza kisha.
41. **TOFA:** Jinamizi! Kwa ufupi hilo ndio naweza kusema kuhusu hiyo ajali. Sijui baya ni lipi, Oluanda kupoteza mguu wake au mimi kumpoteza Oluanda...
42. **THERESA:** Huwezi kumpoteza ; hutampoteza Oluanda.
43. **TOFA:** Siku hizi hasidi wake mkubwa ni mimi, hata Kangwa alifukuzwa. Penzi kubwa kwake ni viatu siku hizi..
44. **THERESA:** (**Surprised**) Viatu?
45. **TOFA:** Viatu eeh!. Mwezi mzima Oluanda alipokuwa yuwauguza mguu wake hakuona ajira nyengine yakufanya ila kunitengezea viatu vyangu vyote vikuukuu..( **Tearful**) alisema kwa vile hatavaa tena viatu basi heri ashone viatu

vyote...

46. **THERESA:** Hmm.. ni kama ambaye historia inajirudia..
47. **TOFA:** Historia gani? Theresa, hakuna ajuae ninayopitia..
48. **THERESA:** Ngoja tupate lishe la mchana kwa sasa; nina mengi yakukueleza . **(Calls out)** Zabibu!... Zabibu!
49. **MSIMULIZI:** Nyanya Theresa bila shaka alihisi anavyohisi Tofa. Zaidi ya hayo alijuwa ni kwa nini Oluanda alijipurukusha na kushona viatu, hata kama hakuwa mahiri wa kazi ya ushonaji viatu. Kule shulenii Oluanda hakuja kitakachoteka alipoitwa afisini kwa mwalimu mkuu.

#### **SCENE FOUR: HEADTEACHER'S OFFICE**

50. **SFX:** GENTLE KNOCK ON DOOR
51. **BI. NINA:** Ingia!
52. **SFX:** DOOR OPENED WITH DIFFICULTY;  
SOUNDS OF CRUTCHES, ROOM  
AMBIENCE
53. **OLUANDA:** Shikamoo Mwalimu mkuu, nimeambiwa umeniita.

54. **BI. NINA:** Ndio keti chini Oluanda.
55. **SFX:** **CHAIR PULLED ASIDE; CRUTCHES BEING SET ASIDE**
56. **OLUANDA:** Asante mwalimu. (**takes a deep breath**)
57. **BI. NINA:** Natumai huna tatizo lolote tangu urudi shule baada ya ajali yako.
58. **OLUANDA:** (**Baffled**) Naam... ni sawa. Nafurahia kurudi shuleni.
59. **BI. NINA:** Oluanda, waalimu wengi wamekuja hapa afisini kwangu,najua itakuwa ngumu kwako lakini kwa manufaa ya wote sina budi ila kukuacha uende nyumbani.
60. **OLUANDA:** (**Shocked**) Lakini kwanini Bi. Nina? Kama ni suala langu la kuchelewa basi nitajibidiisha, hakika nitabidiika; bado najifunza kutumia haya magongo mwalimu.
61. **BI.NINA:** La, Oluanda,sio kuhusu hayo. Sijui nikueleze viyi unielewe vyema? Hatutaki uteseke, pia zipo shule maalum za watu kama nyinyi, mamako anafaa kukusajilisha huko. Wewe ni mwanafunzi mwerevu, lakini hatuna uzoefu na hali yako kwa sasa na hakuna mwalimu ye yeyote ikiwepo mimi anayejuwa jinsi ya kukuhudumia.

62. **OLUANDA:** Bi. Nina hayo ndio nimekua nikimueleza mamangu. Sihitaji huduma yejote maalum. Ndio , matembezi ni shida kidogo kwa hivi sasa, lakini bado nahisi nina nguvu na uwezo wangu kamili kama awali. Hata najifunza kushona viatu.
63. **BI. NINA:** Viatu?... viatu vya nani? Tuache hayo. Oluanda muhimu ni kuwa: hatuwezi kuwa nawe katika shule hii ya wanafunzi kamili. Walimu wamekubaliana, kwa manufaa yako mwenyewe kukuepusha na utundu na kejeli za wanafunzi wengine. Unamjuwa Zabibu, dadake Karemi alipata shida zizo hizo kwa ajili ya kuwa zeruzeru.
64. **OLUANDA:** Lakini mimi ni yule yule, Oluanda. Sijui kwanini nyote munanitenga kama mtu mgeni msiomtambua.
65. **BI. NINA:** Tafadhali mueleze mamako uamuzi wetu na kama ana swali anaweza kuja tujadiliane. Ni hayo.
66. **OLUANDA:** Kwa hiyo nafukuzwa shule,si kwa ajili ya utundu au ukosa adabu, bali kwa ajili ya udhaifu wangu? Ulemavu .. sivyo?
67. **BI. NINA:** Oluanda, usijaaribu kunifanya nihukumike!

Nakuhurumia kweli lakini pia sera ya shule ni muhimu. Kesho usije shule na iwapo utakuja basi njoo na mzazi wako.

**68. SFX: SCHOOL BELL RINGS**

**HITIMISHO:** Baada ya kengele ya shule kupigwa, Oluanda aliyazoazoa magongo yake na kumtazama kwa muda Bi. Nina ambaye kauzika uso wake katika mlima wa vitabu ili kumuepuka Oluanda, walisema : ukitaka kumuua nyani, usimtazame usoni! Kwa haya basi tunatia nanga katika kipindi chetu cha nne hadithi kwa jina “ **Ulemavu barani Afrika**” Sasa Oluanda atakuwa mgeni wa nani? Mamake atazipokea vipi habari hizi? Na Nyanya Theresa kumbuka bado hajamfafanulia Tofa hadithi yake. Kwa haya na mengineyo ni kipindi kifuatacho. Kusikiliza kipindi hiki tena au chenginecho tembelea tovuti zetu

[www.dw-world.de/lbe.mp3](http://www.dw-world.de/lbe.mp3) Nakutakia wakati mufti.